**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

**Anuani ya Simu:** "Kilimo Dodoma"
**Simu:** 022-26 2321407
**Faksi:** 022-26 2320037
**Barua Pepe:** ***ps@kilimo.go.tz***
**Tovuti:** ***www.kilimo.go.tz***

Idara ya Utawala,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P. 2182,
**DODOMA.**

***Unapojibu tafadhali taja:***
**Kumb. Na. BA.12/27/02**

**24 Septemba, 2024**

Katibu mkuu,
Ofisi ya Rais TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
**DODOMA.**

**YAH: MWONGOZO ULIOBORESHWA WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU YA MBOLEA KWA WAKULIMA MSIMU WA 2023/2024**

Tafadhali rejea barua yetu yenye Kumb. Na. BA.12/27/02 ya tarehe 06 Septemba, 2024 kuhusu somo tajwa hapo juu.

2. Kupitia barua hiyo, Wizara ya Kilimo iliiomba OR-TAMISEMI kuusambaza Mwongozo tajwa kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili usambazwe kwa Wadau wote katika ngazi za Mikoa kwa ajili ya utekelezaji.

3. Ili kuweka mazingira ya ufanisi zaidi katika utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima kupitia mfumo wa kidigitali, Wizara imefanya maboresho kidogo katika Mwongozo uliowasilishwa kwako tarehe 06 Septemba, 2024.

4. Kwa barua hii, ninapenda kukufahamisha kwamba Wizara ya Kilimo inafuta Mwongozo huo uliotolewa awali na inaiomba OR-TAMISEMI kuusambaza Mwongozo huu mpya kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili usambazwe kwa wadau wote katika ngazi husika.

Ninakushukuru kwa ushirikiano wako.

Gerald G. Mweli, *ndc*
**KATIBU MKUU**

Nakala: Mkurugenzi Mtendaji,
Chama cha Wafanyabiashara wa Mbegu Tanzania (TASTA),
S.L.P. 15216,
**ARUSHA.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

# MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU YA MBEGU ZA MAHINDI MSIMU WA 2024/2025

**24 SEPTEMBA, 2024**

# YALIYOMO

**YALIYOMO** .......... **iv**
**DIBAJI** .......... **iii**
**1.0 UTANGULIZI** .......... **1**
1.1 Chimbuko la Mwongozo .......... 1
1.2 Lengo la Mwongozo .......... 1
**2.0 UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU** .......... **2**
2.1 Usajili na Uhuishaji wa Taarifa za Wakulima .......... 2
2.2 Usajili wa Wazalishaji/ Waagizaji wa Mbegu za Mahindi .......... 2
2.3 Usajili wa Taarifa za Mawakala wa Mbegu .......... 3
2.4 Bei elekezi ya mbegu za mahindi katika mpango wa ruzuku .......... 3
2.5 Marekebisho ya Bei Kikomo .......... 5
2.6 Usambazaji na Uuzaji wa Mbegu za Mahindi .......... 5
2.7 Utoaji wa Elimu na Mafunzo kwa Wadau .......... 5
2.8 Usimamizi wa Utoaji wa Ruzuku ya Mbegu za Mahindi .......... 5
2.9 Utoaji wa Adhabu .......... 5
2.10 Utaratibu wa malipo ya ruzuku ya mbegu .......... 6
**3.0 MFUMO WA KIDIJITI WA UTEKELEZAJI WA RUZUKU** .......... **6**
3.1 Muundo wa Mfumo wa Kidijiti wa ruzuku ya Mbegu .......... 6
3.2 Mfumo wa Ruzuku ya Mbegu .......... 8
3.3 Muundo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Ruzuku ya Mbegu za Mahindi .......... 9
3.3.1 Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbegu za Mahindi .......... 9
3.3.2 Kamati ya Taifa ya Ufuatiliaji wa Mpango wa Ruzuku .......... 9
3.3.3 Kamati Tendaji (Technical Committee) ya TOSCI .......... 10
**4.0 NGAZI ZA UTEKELEZAJI NA WAJIBU WA WADAU** .......... **11**
4.1 Wizara ya Kilimo .......... 11
4.2 Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) .......... 11
4.3 Sekretarieti za Mikoa .......... 12
4.4 Mamlaka za Serikali za Mitaa .......... 13
4.5 Wazalishaji/Waagizaji wa Mbegu .......... 13
**5.0 UTARATIBU WA KUPOKEA MALALAMIKO** .......... **15**
**6.0 MAMBO YA KUZINGATIA** .......... **15**
**7.0 HITIMISHO** .......... **16**

## DIBAJI

Katika msimu wa kilimo wa 2024/2025, Serikali inatekeleza Mpango wa Ruzuku ya Mbegu za Mahindi zilizothibitishwa Ubora(certified seeds) kwa wakulima kwa kutumia programu maalum ya kidigiti ambayo pia inatumika katika utoaji wa ruzuku ya mbolea ili kusajili wakulima, wazalishaji/ waagizaji wa mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora, mawakala wa pembejeo na kuratibu usambazaji wa mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima na kusimamia malipo ya ruzuku.

Lengo la kutoa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima ni kupunguza gharama ya upatikanaji na kuongeza matumizi ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora ili kuongeza uzalishaji na tija katika zao la mahindi, kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda na pato kwa mkulima. Utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora utazingatia taarifa za usajili wa wakulima na bajeti ya Serikali. Matumizi ya mfumo wa kidijiti katika kutoa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima yatapunguza mianya ya udanganyifu na kuimarisha usimamizi.

Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Kuthibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (Tanzania Official Seed Certification Institute - TOSCI) itakuwa na jukumu la kuratibu utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora na itaainisha orodha ya aina za mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora zitakazohusika kwenye mpango wa ruzuku. Katika mpango wa ruzuku mkulima atanunua mbegu za mahindi zilizoidhinishwa ubora kwa bei ya ruzuku kulingana na ukubwa wa shamba lake la mahindi.

Mwongozo huu umeainisha wadau mbalimbali na wajibu wao katika kufanikisha utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima kwa msimu wa 2024/2025. Wadau hao ni pamoja na Wizara ya Kilimo, TOSCI, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wazalishaji/Waagizaji wa Mbegu, Mawakala (Agrodealers) wa Mbegu, Taasisi za Fedha, Wakulima wa zao la mahindi na wadau wengine muhimu.

Nitoe wito kwa wadau wa sekta ya kilimo nchini kutumia mwongozo huu kikamilifu kwa lengo la kutambua wajibu wa kila mdau katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Gerald G. Mweli, *ndc*
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA KILIMO**

## 1.0 UTANGULIZI

Katika msimu wa 2024/2025, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inatekeleza mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima kwa lengo la kupunguza gharama ya upatikanaji na kuongeza matumizi ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora ili kuongeza uzalishaji na tija katika zao la mahindi, kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda na Pato kwa mkulima. Zao la mahindi ni miongoni mwa mazao ya chakula ambayo yanalimwa kwa wingi nchini Tanzania, takwimu za uzalishaji wa zao la mahindi zimeonesha uwepo wa ongezeko la uzalishaji kutoka tani 7,039,000 mwaka 2020/2021 hadi kufikia tani 8,010,949 mwaka 2022/2023. Utekelezaji wa Mpango huu wa ruzuku ya mbegu bora ya mahindi unalenga kuhamasisha wakulima wa Tanzania kuongeza uzalishaji wa mahindi kwa kuwezesha utoaji wa tani 52,000 za mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima katika mikoa yote nchini.

### 1.1 Chimbuko la Mwongozo

Chimbuko la Mwongozo ni uwepo wa mpango wa Serikali wa kutoa ruzuku ya mbegu bora ya mahindi kwa wakulima ili kuwawezesha kununua na kutumia mbegu bora katika uzalishaji wa wa zao la mahindi.

### 1.2 Lengo la Mwongozo

Mwongozo huu umelenga kutoa utaratibu wa utekelezaji wa utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima katika msimu wa mwaka 2024/2025. Vilevile, Mwongozo umeainisha wadau mbalimbali na wajibu wao katika usajili, ufuatiliaji na usimamizi na utoaji wa ruzuku ili kufanikisha lengo la Serikali la kutoa ruzuku ya mbegu bora kwa wakulima wa zao la mahindi nchini.

## 2.0 UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU

### 2.1 Usajili na Uhuishaji wa Taarifa za Wakulima

Usajili wa wakulima watakaonufaika na Ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora utafanyika kupitia taratibu za usajili wa wakulima kwenye daftari maalum ambalo linatumika kusajili wakulima katika ngazi za vijiji kwa ajili ya ruzuku ya mbolea. Usajili huo utahusisha hatua mbili ambazo ni usajili kwenye daftari maalum na upandishaji wa taarifa za wakulima kwenye mfumo wa kidijiti unaotumika pia katika utoaji wa ruzuku ya mbolea. Wanufaika wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora ni mkulima mmoja mmoja, vikundi vya wakulima vilivyosajiliwa, Vyama vya Ushirika, Taasisi na Kampuni zinazoendesha kilimo cha mashamba makubwa baada ya kusajiliwa na kupata namba maalum ya utambulisho kutoka kwenye mfumo.

Mfumo wa usajili wa wakulima utahuishwa ili wakulima waliokwisha sajiliwa kwenye mfumo wa ruzuku ya mbolea na kupewa namba maalum ya mkulima, watambulike na kutumia namba hiyo hiyo kununua mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa utaratibu wa ruzuku.

Ili mkulima aweze kusajiliwa anapaswa kuwa na namba yake ya simu wakati wa usajili na simu hiyo ndiyo itatumika kupokea namba ya utambulisho wa mkulima atakayotumia kununua mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora. Mkulima hataruhusiwa kutumia namba ya simu ya mtu mwingine wakati wa usajili au wakati wa kununua mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora.

### 2.2 Usajili wa Wazalishaji/ Waagizaji wa Mbegu za Mahindi

Wazalishaji/Waagizaji wa mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora (certified seeds) watakaoshiriki katika usambazaji wa mbegu za ruzuku watapaswa kufuata hatua zifuatazo:-

i. Kujisajili kwa ajili ya kushiriki kwenye mpango wa ruzuku. Ili kujisajili wazalishaji/waagizaji wa mbegu wanatakiwa kuwasilisha taarifa zifuatazo:-
    a) Hati ya usajili wa TOSCI inayomruhusu kufanya biashara ya mbegu; na
    b) Taarifa za Akaunti ya Benki itakayotumika kwa ajili ya malipo ya ruzuku.

ii. Kuwasilisha TOSCI taarifa za mawakala wake na vituo vya usambazaji wa mbegu kwa wakulima katika kila Mkoa au Wilaya wanakotoa huduma;

iii. TOSCI itachambua maombi na kutoa mrejesho kwa mwombaji; na

iv. Iwapo mwombaji atakuwa amekidhi vigezo atasajiliwa na kupewa namba maalum ya utambulisho na kusaini mkataba utakaoandaliwa na TOSCI.

## 2.3 Usajili wa Taarifa za Mawakala wa Mbegu

Usajili wa mawakala utafanywa na TOSCI kwa kuzingatia orodha iliyowasilishwa na wazalishaji/waagizaji wa mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora. Mawakala watakaoshiriki kusambaza mbegu hizo kwa mpango wa ruzuku watapaswa kufuata hatua zifuatazo:-

i) Kujisajili kushiriki mpango wa ruzuku ambapo watatakiwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-
   a) Awe na hati ya usajili wa TOSCI inayomruhusu kufanya biashara ya mbegu; na
   b) Awe ameteuliwa na kampuni ya mbegu (wazalishaji/waagizaji) kwa ajili ya kusambaza na kuuza mbegu katika mpango wa ruzuku;

ii) Kuhuisha taarifa zake zilizosajiliwa kwenye mfumo msimu wa 2023/2024; na

iii) Kuainisha vituo vya mauzo ya mbegu zilizothibitishwa ubora katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Kijiji.

## 2.4 Bei elekezi ya mbegu za mahindi katika mpango wa ruzuku

Bei elekezi ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa msimu wa kilimo husika itatolewa na TOSCI. Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na TOSCI, bei elekezi kwa msimu wa 2024/2025 itaanza kutumika tarehe 01 Septemba, 2024. Aidha, kwa mbegu za aina mbalimbali za mahindi zilizothibitishwa ubora, bei kikomo ya ruzuku imeainishwa katika **Jedwali Na. 1** kama ifuatavyo:

**Jedwali Na.1**: Bei Kikomo ya Ruzuku ya Aina za Mbegu za Mahindi

| Kundi | | Na. | Aina ya mbegu | Uzito (Kilo) | Bei kikomo yenye ruzuku |
|---|---|---|---|---|---|
| I | Aina za Mbegu zinazochavushwa huria (OPVs) | 1. | NATA K 6Q | 2 | 7,000 |
| | | 2. | NATA K 8 | 2 | 7,000 |
| | | 3. | TZM 523 | 2 | 7,000 |
| | | 4. | LISHE K1 | 2 | 7,000 |
| | | 5. | Bora | 2 | 7,000 |
| | | 6. | TMV-2 | 2 | 7,000 |
| | | 7. | SITUKA M1 | 2 | 7,000 |
| | | 8. | Kilima | 2 | 7,000 |
| | | 9. | Staha | 2 | 7,000 |
| | | 10. | TMV - 1 | 2 | 7,000 |
| | | 11. | T105 | 2 | 7,000 |
| | | 12. | T104 | 2 | 7,000 |
| II | Aina za Mbegu chotara (Hybrid) zinazokomaa mapema na muda wa kati | 1. | NATA H 105 | 2 | 14,000 |
| | | 2. | UH 6303 | 2 | 14,000 |
| | | 3. | UH 615 | 2 | 14,000 |
| | | 4. | DK 8031 | 2 | 14,000 |
| | | 5. | DKC 80-33 | 2 | 14,000 |
| | | 6. | DKC 80-53 | 2 | 14,000 |
| | | 7. | SY 6444 | 2 | 14,000 |
| | | 8. | SY 5054 | 2 | 14,000 |
| | | 9. | PAN-3M-05 | 2 | 14,000 |

| Kundi | | Na. | Aina ya mbegu | Uzito (Kilo) | Bei kikomo yenye ruzuku |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 10. | 30G19 | 2 | 14,000 |
| | | 11. | P 3812 W | 2 | 14,000 |
| | | 12. | PAN 15 | 2 | 14,000 |
| | | 13. | PAN 3M-05 | 2 | 14,000 |
| | | 14. | PAN 53 | 2 | 14,000 |
| | | 15. | PAN 4M-19 | 2 | 14,000 |
| | | 16. | PHB 3253 | 2 | 14,000 |
| | | 17. | ETG M 601 | 2 | 14,000 |
| | | 18. | Kaspidi | 2 | 14,000 |
| | | 19. | Lubango | 2 | 14,000 |
| | | 20. | H 513 | 2 | 14,000 |
| | | 21. | DH 04 | 2 | 14,000 |
| | | 22. | H 625 | 2 | 14,000 |
| | | 23. | H 628 | 2 | 14,000 |
| | | 24. | H 614 | 2 | 14,000 |
| | | 25. | MAMSH 457 | 2 | 14,000 |
| | | 26. | WE4102 | 2 | 14,000 |
| | | 27. | MAMSH 458 | 2 | 14,000 |
| | | 28. | MERU VAH 517 | 2 | 14,000 |
| | | 29. | MERU VAH 519 | 2 | 14,000 |
| | | 30. | MERU HB 405 | 2 | 14,000 |
| | | 31. | MERU HB 513 | 2 | 14,000 |
| | | 32. | MERU HB 623 | 2 | 14,000 |
| | | 33. | WE 4114 | 2 | 14,000 |
| | | 34. | SC 303 | 2 | 14,000 |
| | | 35. | SC 403 | 2 | 14,000 |
| | | 36. | SC 419 | 2 | 14,000 |
| | | 37. | SC 513 | 2 | 14,000 |
| | | 38. | SC 555 | 2 | 14,000 |
| | | 39. | SC 657 | 2 | 14,000 |
| | | 40. | TZH 536 | 2 | 14,000 |
| | | 41. | TZH 538 | 2 | 14,000 |
| | | 42. | KH 500-43A | 2 | 14,000 |
| | | 43. | EAS401 | 2 | 14,000 |
| | | 44. | WH 509 | 2 | 14,000 |
| | | 45. | WH 605 | 2 | 14,000 |
| | | 46. | WH 403 | 2 | 14,000 |
| | | 47. | WH 505 | 2 | 14,000 |
| | | 48. | ZMS 606 | 2 | 14,000 |
| | | 49. | ZMS 405 | 2 | 14,000 |
| | | 50. | ZMS 402 | 2 | 14,000 |
| | Aina za Mbegu Chotara (Hybrid) zinazokomaa kwa muda mrefu | 1. | DK 777 | 2 | 14,500 |
| | | 2. | DKC 90-89 | 2 | 14,500 |
| | | 3. | PAN691 | 2 | 14,500 |
| | | 4. | SC 719 | 2 | 14,500 |
| | | 5. | ZMS 638 | 2 | 14,500 |

## 2.5 Marekebisho ya Bei Kikomo

TOSCI inaweza kufanya marekebisho ya Jedwali Na. 1 kuhusu bei kikomo ya aina ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora iwapo kutakuwa na aina nyingine ya mbegu ya mahindi au mbegu mpya itakayosajiliwa, kufanyiwa tathmini na kuainishwa kwa bei ya ukomo. Wazalishaji/waagizaji wa mbegu za mahindi wanaweza kuwasilisha maombi kwa TOSCI ya kusambaza mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora ili kujumuishwa kwenye Mpango wa Ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora.

## 2.6 Usambazaji na Uuzaji wa Mbegu za Mahindi

Usambazaji na uuzaji wa mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima utafanywa na kampuni za mbegu na mawakala wao au Vyama vya Ushirika watakao sajiliwa kwenye mfumo wa kidijiti wa ruzuku.

Kampuni au Vyama vya Ushirika watapaswa kuhakikisha kwamba mawakala wao wana mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora katika kipindi chote cha msimu wa kilimo ili kukidhi mahitaji ya wakulima.

## 2.7 Utoaji wa Elimu na Mafunzo kwa Wadau

Utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima utahusisha utoaji wa elimu na mafunzo kwa wadau mbalimbali watakaoshiriki katika mpango wa ruzuku. Kila ngazi ya utekelezaji ina jukumu la kutoa elimu kwa wadau kuhusu mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi kwa wakulima ili kujenga uelewa namna ruzuku inavyotolewa.

## 2.8 Usimamizi wa Utoaji wa Ruzuku ya Mbegu za Mahindi

Kuhusu usimamizi wa mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora utahusisha Wizara ya Kilimo kutenga bajeti ya kugharamia ruzuku na kuunda kamati itakayofanya ufuatiliaji na tathimini ya mpango huo. Majukumu hayo kwa Wizara ya Kilimo yatatekelezwa kwa kushirikiana na TOSCI na TFRA, na OR-TAMISEMI yatahusisha Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## 2.9 Utoaji wa Adhabu

Utekelezaji wa Mwongozo huu utazingatia Sheria za nchi na Kanuni zake, ikiwa ni pamoja na Sheria ya mbegu, Sura ya 308 na Kanuni za Sheria hiyo. Pia, utekelezaji huo utazingatia taratibu zilizowekwa au zitakazowekwa kwa kuzingatia Sera ya Kilimo au vipaumbele vya Wizara ya Kilimo kwa msimu husika. Hatua hizo zinakusudia kuhakikisha wadau katika tasnia ya mbegu wanatekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Mwongozo huu na kuhakikisha kuwa wakulima wananufaika na mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora pamoja na kuchukua hatua za kisheria, kiutawala na kinidhamu kwa yeyote atakayekiuka utekelezaji wa mwongozo au maelekezo yatakayotolewa kuhususiana na mwongozo huu.

Aidha, mdau atakayekiuka utaratibu ulioainishwa katika mwongozo huu kwa kukusudia, kufanya uzembe utakaosababisha hasara au kutotekelezwa kwa mwongozo huu ipasavyo au kujinufaisha atachukuliwa hatua za kisheria na endapo atatiwa hatiani na mahakama yenye mamlaka, atapewa adhabu kwa mujibu wa Sheria husika za nchi, ikiwa ni pamoja na Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329; na Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200.

## 2.10 Utaratibu wa malipo ya ruzuku ya mbegu

Aina mbalimbali za mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora zitasambazwa kwa wakulima na wazalishaji/waagizaji,Vyama vya Ushirika au mawakala wao waliosajiliwa kwenye mfumo wa ruzuku kwa kuwasilisha madai ya huduma walizozitoa kwa wakulima kwa utaratibu ufuatao:-


i) Kampuni ya mbegu itaandaa hati ya madai kwa mbegu zilizouzwa kwa wakulima na kuwasilisha TOSCI kupitia mfumo wa kidijiti wa ruzuku. Hati hiyo iambatishwe na *Delivery Note*, risiti ya kielekitroniki (**EFD receipt**), orodha ya wakulima walionunua mbegu, aina ya mbegu na kiasi cha mbegu zilizonunuliwa, vituo vya mauzo na barua ya maombi ya malipo;
ii) TOSCI itahakiki na kuidhinisha malipo ya fedha ya ruzuku kwa Kampuni husika baada ya kupokea hati ya madai na kufanya usuluhishi (reconciliation) wa huduma iliyotolewa; na
iii) Malipo yatafanyika kwa kuzingatia bei elekezi ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa aina husika kama ilivyoainishwa kwenye kipengele cha 2.4.

## 3.0 MFUMO WA KIDIJITI WA UTEKELEZAJI WA RUZUKU

## 3.1 Muundo wa Mfumo wa Kidijiti wa ruzuku ya Mbegu

Utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa mwaka wa 2024/2025, utatumia programu maalum ya kidijiti unaotumika pia katika utoaji wa ruzuku ya mbolea (**Digital Fertilizer Subsidy Distribution and Payment System**). Mfumo huo, utatumika kusajili au kuhakiki taarifa za wadau muhimu wakiwemo wakulima, wazalishaji na waagizaji wa mbegu, mawakala wa mbegu na kufanya malipo kwa kampuni za mbegu zilizotoa huduma. Vilevile, Mfumo utahusisha ushiriki wa Wizara ya Kilimo, Taasisi za Kifedha na TOSCI. Muundo wa Mfumo wa Kidijiti wa Ruzuku ya Mbegu za Mahindi umeainishwa kwenye kipengele cha 3.3.

Muundo wa Mfumo wa Kidijiti wa Ruzuku ya Mbegu za Mahindi Zilizothibitishwa Ubora utakuwa kama ifuatavyo:-



## 3.2 Mfumo wa Ruzuku ya Mbegu

Mfumo wa kidijitali utakaotumika katika utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa msimu wa 2024/2025, utazingatia utaratibu ufuatao:-

i) Wazalishaji/waagizaji wa mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora waliosajiliwa kwa mujibu wa mwongozo na utaratibu wa usajili watapewa namba za utambulisho kuthibitisha ushiriki wao, sambamba na namba hizo watapewa uwezo wa kuingia kwenye mfumo kupitia kurasa zao (**portal**);

ii) Wazalishaji/waagizaji wa mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora watasambaza mbegu kwenye vituo vya mauzo na mawakala waliosajiliwa. Zoezi hilo litahusisha utoaji na upokeaji wa kiasi cha mbegu kwenye mfumo (stock in and out). Kiasi cha mbegu (Stock) kitakachotolewa kwenye maghala husika kwenda kwenye vituo vya mauzo kitafuatiliwa kuanzia ngazi ya TOSCI hadi kwa mkulima;

iii) Wazalishaji/ Waagizaji, Mawakala na vituo vyote vya mauzo havitaruhusiwa kuuza mbegu za mahindi nje ya utarajibu wa ruzuku;

iv) Mkulima aliyesajiliwa na kuhakikiwa taarifa zake ataenda kwa Wakala/Kituo cha usambazaji wa mbegu na kuonesha namba ya utambulisho ili aweze kununua mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kupitia mfumo wa ruzuku;

v) Mfanyabiashara/wakala ataingiza namba ya utambulisho wa mkulima kwenye mfumo na kuhakiki taarifa (Jina kamili, eneo analotoka, ukubwa wa shamba, idadi ya mifuko ya mbegu bora anayopaswa kulipia kwa wakati huo) kabla ya kumuuzia mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora;

vi) Baada ya namba ya mkulima kwenye mfumo, mfanyabiashara/wakala ataskani *QR code* kwa mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora zinazouzwa na taarifa za mbegu hizo (aina, kampuni na namba ya mfuko) zitaingia kwenye mfumo wa kidijitali;

vii) Mkulima atapokea meseji fupi nyenye namba ya siri ya muda *(One Time Password- OTP)* ambayo itatumika ndani ya dakika tano. Mkulima atampa mfanyabiashara/wakala namba hiyo ya *OTP* ili kuthibitisha manunuzi ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kufanyika;

viii) Baada ya kuthibitisha, mfumo utamruhusu wakala kumalizia taratibu za kumuuzia mkulima mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora;

ix) Mkulima atamlipa mfanyabiashara/wakala fedha taslimu kwa ajili ya kiasi cha mbegu bora anachohitaji kununua kwa kuzingatia bei elekezi iliyotangazwa na Serikali;

x) Wakala atatoa risiti ya EFD kwa mkulima baada ya kupokea malipo;

xi) Taarifa za mauzo zitaonekana kwenye ukurasa (portal) wa Wazalishaji/Waagizaji husika na TOSCI;

xii) Wazalishaji/Waagizaji watawasilisha hati ya madai TOSCI kulingana na kiasi cha mbegu bora ambacho kimeuzwa kwa wakulima;

xiii) TOSCI itahakiki madai yaliyowasilishwa na kuidhinisha malipo ya fedha ya ruzuku kwa Wazalishaji/waagizaji husika; na

xiv) Malipo kwa Wazalishaji/waagizaji yatafanyika kwa kuzingatia taratibu za malipo ya Serikali.

## 3.3 Muundo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Ruzuku ya Mbegu za Mahindi

### 3.3.1 Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbegu za Mahindi

Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora (*National Subsidy Steering Committee)* itakuwa na wajumbe wafuatao: -

| | |
|---|---|
| Waziri wa Kilimo | Mwenyekiti |
| Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo | Mjumbe |
| Katibu Mkuu Wizara ya Fedha | Mjumbe |
| Katibu Mkuu OR- TAMISEMI | Mjumbe |
| Mwakilishi wa kampuni za Mbegu Tanzania (TASTA) | Mjumbe |
| Mkurugenzi wa Sera na Mipango – Wizara ya Kilimo | Mjumbe |
| Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Mazao | Mjumbe |
| Mkurugenzi Tawala za Mikoa- OR-TAMISEMI | Mjumbe |
| Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya TOSCI | Sekretarieti |
| Mkurugenzi Mkuu TOSCI | Katibu |

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo anaweza kualika mdau yoyote kushiriki kikao cha kamati hii kulingana na agenda za kikao husika. Majukumu ya Kamati ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora yatakuwa:-

i) Kuidhinisha vigezo vitakavyotumika kutoa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima;
ii) Kuhakikisha kuwa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora unapata fedha na zinatolewa kwa wakati;
iii) Kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora; na
iv) Kutoa maelekezo mahsusi kwa ajili ya kufanikisha lengo la Serikali la utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima.

### 3.3.2 Kamati ya Taifa ya Ufuatiliaji wa Mpango wa Ruzuku

Kamati ya Taifa ya Ufuatiliaji wa Mpango wa Ruzuku itaundwa na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo. Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wasiozidi kumi (10) ambao watakuwa na majukumu yafuatayo:-

i) Kufuatilia utekelezaji wa mpango wa ruzuku katika Mikoa na Halmashauri za Wilaya;
ii) Kuhakiki kanzidata ya wakulima waliosajiliwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
iii) Kufuatilia mwenendo wa uuzaji na matumizi ya mbegu kwa wakulima;
iv) Kutathmini taarifa za utekelezaji zinazotolewa na TOSCI, Mikoa na Halmashauri za Wilaya na kuiwasilisha kwa Kamati ya Taifa ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku (National Subsidy Steering Committee); na

v) Kubaini changamoto zilizopo na kuzipatia ufumbuzi kwa kushauriana na Wizara ya Kilimo, Sekeretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku.

### 3.3.3 Kamati Tendaji (Technical Committee) ya TOSCI

Kamati Tendaji itasimamia utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora na itaundwa na Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI. Kamati hii itakuwa na Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wasiozidi kumi (10) na itakuwa na majukumu yafuatayo:-

i) Kusajili makampuni na wafanyabishara wa mbegu watakaoshiriki katika mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora;
ii) Kutoa elimu ya mfumo wa ruzuku ya mbegu za mahindi kwa wadau;
iii) Kuratibu uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora;
iv) Kuwa sekretarieti ya Kamati ya Taifa ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku;
v) Kuratibu shughuli za uhamasishaji wa mpango wa ruzuku (*program promotion*) ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora;
vi) Kuratibu shughuli za ufuatiliaji na tathmini; na
vii) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu bora kwa mwezi, robo mwaka, nusu mwaka, na mwaka na kuiwasilisha kwenye Kamati ya Taifa ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku (National Subsidy Steering Committee).

## 4.0 NGAZI ZA UTEKELEZAJI NA WAJIBU WA WADAU

Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora unahusisha ngazi mbalimbali za utekelezaji na majukumu yake. Ngazi zitakazohusika katika mpango wa ruzuku ni Wizara ya Kilimo, TOSCI, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wazalishaji/waagizaji wa mbegu, Mawakala wa mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora, Taasisi za Fedha na Wakulima. Vyombo/taasisi mbalimbali vitakuwa na majukumu tofauti ya utekelezaji.

### 4.1 Wizara ya Kilimo

Majukumu ya Wizara ya Kilimo yatakuwa ni:-

i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora;
ii) Kufuatilia upatikanaji wa fedha za ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora;
iii) Kuunda Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku (National Subsidy Steering Committee) na Kamati ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathimini ya Mpango wa Ruzuku;
iv) Kutoa Mwongozo wa Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbegu kwa wadau;
v) Kutoa maelekezo yatakayowezesha utekelezaji wa mpango wa ruzuku;
vi) Kushughulikia masuala mengine yatakayohitaji maamuzi ya Wizara; na
vii) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji ili kuhakikisha kuwa mpango wa ruzuku unatekelezwa kwa mujibu wa Mwongozo uliotolewa.

### 4.2 Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI)

Majukumu ya TOSCI yatakuwa ni:-

i) Kusajili Wazalishaji/waagizaji wa mbegu, mawakala na vituo vya mauzo ya mbegu zilizothibitishwa ubora;
ii) Kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kutambua wakulima watakaonufaika na ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kupitia Mfumo wa ruzuku ya mbolea;
iii) Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa kutumia mfumo unaotumika kutoa ruzuku ya Mbolea;
iv) Kuunda Kamati Tendaji kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora;
v) Kuingia mikataba ya makubaliano na wazalishaji/waagizaji wa mbegu waliosajiliwa kwa ajili ya kuuza mbegu kwa wakulima katika mpango wa ruzuku;
vi) Kuingia mikataba na watoa huduma mbalimbali katika utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbegu;
vii) Kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Kilimo, kupanga na kutangaza bei elekezi ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora na kusimamia utekelezaji wake;

viii) Kushirikiana na wadau wa mbegu katika kufanikisha utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora;
ix) Kutoa elimu kwa umma kuhusu utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine muhimu;
x) Kufungua na kusimamia akaunti maalum zitakazotumika kupokea na kulipa fedha za ruzuku kwa watoa huduma;
xi) Kuidhinisha malipo ya ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora iliyouzwa kwa wakulima;
xii) Kushirikiana na Taasisi za Fedha kufanya usuluhishi wa malipo ya ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora mara kwa mara;
xiii) Kutoa adhabu na faini ikiwemo kumsimamisha kwenye mfumo mfanyabiashara/mkulima atakayebainika kufanya udanganyifu kinyume na taratibu zilizoainishwa kwenye Mwongozo huu au kwenda kinyume na Sheria za nchi ikiwemo Sheria ya Mbegu Sura 308 na Kanuni zake;
xiv) Kupokea na kushughulikia malalamiko/changamoto za utekelezaji zinazohusu mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora na kuwasilisha taarifa Wizara ya Kilimo;
xv) Kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima; na
xvi) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kila mwezi na kuiwasilisha Wizara ya Kilimo.

## 4.3 Sekretarieti za Mikoa

Majukumu ya Sekretarieti za Mikoa yatakuwa ni:-

i) Kusimamia Halmashauri zote zilizopo kwenye mikoa husika ili zitekeleze kwa ufanisi majukumu yake kwa mujibu wa mwongozo wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora;
ii) Kushirikiana na TOSCI katika kuhamasisha wakulima kujisajili katika daftari la mkulima kwenye ngazi ya vijiji ili taarifa zao ziingizwe kwenye mfumo wa kidigiti na kuwezesha kupatikana kwa namba maalum za wakulima zitakazotumika kununulia mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa bei ya ruzuku;
iii) Kufuatilia utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora katika kila Halmashauri zilizopo kwenye mkoa husika; na
iv) Kuhamasisha wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo kufungua vituo vya mauzo ya mbegu bora katika maeneo ya uzalishaji;
v) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kila mwezi na kuiwasilisha Wizara ya Kilimo na TOSCI.

### 4.4 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yatakuwa ni : -

i) Kuhamasisha matumizi ya mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora katika kuongeza uzalishaji wa zao la mahindi;
ii) Kushirikiana na TOSCI katika kuhamasisha wakulima kujisajili katika daftari la mkulima kwenye ngazi ya vijiji ili taarifa zao ziingizwe kwenye mfumo wa kidigiti na kuwezesha kupatikana kwa namba maalum za wakulima zitakazotumika kununulia mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa bei ya ruzuku;
iii) Kuhamasisha wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo kufungua vituo vya mauzo ya mbegu bora katika maeneo ya uzalishaji;
iv) Kusajili wakulima kwenye mfumo wa kidigiti kwa kuingiza taarifa za wakulima zilizoainishwa kwenye daftari la mkulima katika ngazi ya kijiji/mtaa;
v) Kusimamia usambazaji wa mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa wakulima kwa kuzingatia bei elekezi zitakazotangazwa na Serikali;
vi) Kupokea maoni kutoka kwa wafanyabiashara wa mbegu kuhusu hali ya usambazaji wa mbegu za ruzuku na kutoa mapendekezo kwa TOSCI pale inapotokea changamoto za usambazaji;
vii) Kutoa elimu kwa wadau wote kwenye ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora; na
viii) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kila mwezi na kuiwasilisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

### 4.5 Wazalishaji/Waagizaji wa Mbegu

Kampuni zinazojihusisha na uzalishaji na uagizaji wa mbegu zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

i) Kujisajili kushiriki katika mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi;
ii) Kuingiza nchini au kuzalisha mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora zitakazouzwa kwa bei ya ruzuku kwa wakulima;
iii) Kusaini mikataba ya utoaji wa huduma ya uuzaji wa mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora katika mpango wa ruzuku;
iv) Kuwasilisha TOSCI orodha ya mawakala watakaofanya nao kazi ya usambazaji wa mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora;
v) Kuingia mikataba na wafanyabiashara/mawakala wa kusambaza mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kupitia mfumo wa ruzuku;
vi) Kuingiza kwenye mfumo wa kidijitali taarifa za mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora zilizozalishwa/kuagizwa nje ya nchi na kusambazwa kwenye vituo vya mauzo au kuuzwa kwa wakala kupitia mpango wa ruzuku;
vii) Kuhakikisha mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora zinafungashwa katika mifuko ambayo imeandikwa "**MBEGU ZA RUZUKU**"
viii) Kuwasimamia mawakala waliowateua ili kuhakikisha wanafikisha na kuuza mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa wakulima kwa kufuata utaratibu uliowekwa;

ix) Kuwasilisha hati za madai ya fedha za ruzuku kwa TOSCI baada ya kusambaza na kuuza mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora za ruzuku kwa wakulima; na
x) Kuhakikisha mawakala walioingia nao mikataba wanakuwa na mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora wakati wote wa msimu.

### 4.6 Mawakala (Agrodealers) wa Mbegu

Majukumu ya Mawakala (Agrodealers) wa mbegu yatakuwa ni:-

i) Kuingia mkataba na wazalishaji/waagizaji wa mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa ajili ya kushiriki katika mpango wa ruzuku ya utoaji wa mbegu za mahindi kwa wakulima;
ii) Kuhakikisha wanaanzisha vituo vya mauzo karibu na maeneo ya uzalishaji ili kupunguza umbali wa kufuata mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora;
iii) Kutumia mfumo wa kidijiti wa ruzuku ya mbolea unaoratibiwa na TFRA katika kuuza mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa mkulima aliyesajiliwa;
iv) Kutoa taarifa kwa TOSCI kuhusu viashiria vya udanganyifu vinavyojitokea wakati wa kuuza mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora; na
v) Kuhakikisha mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora za ruzuku zinasambazwa na kuuzwa kwa wakulima kwa bei ya ruzuku wakati wote wa msimu wa 2024/2025.

### 4.7 Taasisi za Fedha

Majukumu ya Taasisi za Fedha yatakuwa ni:-

i) Kupokea fedha za ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kutoka Serikalini kupitia akaunti maalum kwa ajili ya kuwezesha malipo yanayostahili kwa watoa huduma;
ii) Kufanya malipo kwa kampuni za mbegu zilizotoa huduma ya kuuza mbegu za mahindi za ruzuku kwa wakulima baada ya kupata idhini ya TOSCI; na
iii) Kushirikiana na TOSCI kufanya usuluhishi wa malipo ya ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora mara kwa mara.

### 4.8 Wakulima

Majukumu ya wakulima watakaonufaika na ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora yatakuwa ni:-

i) Kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye daftari la mkulima ili kupata namba maalum itakayotumika kununulia mbolea na mbegu za ruzuku;
ii) Kuhakiki taarifa zake kwenye daftari la mkulima ili kuwezesha kupewa ruzuku kulingana na takwimu sahihi za mashamba na aina ya mazao anayolima;
iii) Kutunza namba ya utambulisho ya ruzuku ya mbegu ili kutumika katika ununuzi wa mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa utaratibu wa ruzuku;
iv) Kuonesha namba ya utambulisho aliyopewa wakati wa usajili anapokwenda kununua mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa wakala;

v) Kuthibitisha manunuzi ya mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa kutoa namba ya siri (One Time Password - OTP) kwa wakala anaponua mbegu za ruzuku;
vi) Kununua mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa bei elekezi iliyotangazwa na Serikali; na
vii) Kutoa taarifa kwa Mamlaka pale anapohisi kuna viashiria vya udanganyifu.

**ANGALIZO:** Namba ya Mkulima inayotumika kununulia mbolea ya ruzuku ni namba ileile ambayo inatumika katika ununuzi wa mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa utaratibu wa ruzuku. Hivyo, kwa wakulima waliokwishasajiliwa kwenye mfumo wa kidigiti wa mbolea ya ruzuku na kupewa namba ya mkulima watatumia namba hiyo hiyo kununulia mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa utaratibu wa ruzuku.

## 5.0 UTARATIBU WA KUPOKEA MALALAMIKO

Mwongozo huu unaweka utaratibu wa kupokea na kushungulikia malalamiko yanayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa mpango wa utoaji wa ruzuku kwa aina mbalimbali ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kama ifuatavyo:-

i) Mfaidika wa Mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kabla ya kuwasilisha malalamiko yake TOSCI, atapaswa kuwasilisha malalamiko yake kwa maandishi kwa mdau aliyempatia huduma husika na nakala kwa Afisa Kilimo wa Kijiji au Kata husika. Mtoa huduma atatakiwa kutoa majibu/ufafanuzi kwa mlalamikaji katika kipindi cha siku 21 tangu tarehe ya kupokea malalamiko hayo na nakala kwa Afisa Kilimo wa Kijiji au Kata husika ambaye ataingilia kati na kusuluhisha au kupendekeza hatua stahiki zinazoweza kuchukuliwa;

ii) Endapo mtoa huduma hatashughulikia malalamiko hayo kwa kipindi tajwa hapo juu, mlalamikaji anaweza kuwasilisha malalamiko yake TOSCI kwa maandishi akiambatisha pamoja na barua ya malalamiko aliyoiwasilisha kwa mtoa huduma husika;

iii) Baada ya TOSCI kupokea malalamiko hayo itafanya ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na mtoa huduma aliyelalamikiwa na kutatua malalamiko hayo katika kipindi cha siku 45 au kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria za nchi;

iv) Mfaidika wa Mpango wa Ruzuku hii ambaye malalamiko yake hayatapatiwa ufumbuzi na TOSCI kama ilivyoainishwa hapo juu, anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa Wizara ya Kilimo kwa maandishi akiainisha jambo analolilalamikia na kuambatisha barua ya malalamiko yake ya awali kwa TOSCI na Wizara itafanya ufuatiliaji na kutoa ushauri au maelekezo au kuchukua hatua stahiki.

## 6.0 MAMBO YA KUZINGATIA

Wadau wote wanapaswa kuzingatia masuala yafuatayo:-

i) Kila mkulima anapaswa kujisajili kwenye mfumo ili kupata namba ya kununulia mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora kwa utaratibu wa ruzuku;

ii) Kila mkulima anapaswa kutunza namba yake ya kununulia mbegu/mbolea na haitaruhusiwa kutumiwa na mkulima mwingine;

iii) Mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa msimu wa 2024/2025 utafikia ukomo tarehe 30 Juni, 2025

iv) Mtoa huduma ataainisha mawasiliano yake katika kituo cha mauzo kwa kuainisha majina ya kampuni ya mbegu/wakala/ chama cha ushirika, sanduku la posta/namba ya nyumba ya eneo la biashara/mtaa, namba ya simu au anuani ya barua pepe ili kuwezesha mawasiliano kati yake na wateja/wanufaika wa mpango wa ruzuku;

v) Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kubaini changamoto zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi;

vi) Wadau wanaweza kupata ushauri wa kiutaalam kupitia wataalama wa kilimo waliopo katika ngazi ya Wilaya, Kata, Kijiji/Mtaa au kupiga simu katika Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Wizara ya Kilimo kupitia namba 0733 800 200 na 0800 110 153/4 kuanzia saa 1:30 Asubuhi hadi saa 4:00 Usiku;

vii) Kuzingatia utaratibu wa kuwasilisha madai ya malipo kwa huduma zilizotolewa kwa wakulima; na

viii) Kuzingatia utaratibu wa ushughulikiaji wa malalamiko kama ilivyoainishwa katika Kipengele cha 5 cha Mwongozo huu.

## 7.0 HITIMISHO

Serikali imeamua kutoa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa wakulima ili kuwaongezea uwezo wa kununua na kutumia mbegu bora kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija, kuimarisha uhakika wa chakula na kuongeza kipato cha wakulima. Hivyo basi, ni wajibu wa wadau wote kutekeleza majukumu yao kikamilifu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali inahimiza ushirikiano wa wadau katika ngazi zote ili kuhakikisha kuwa mpango wa ruzuku wa mbegu za mahindi zilizothibitihwa ubora unatekelezwa kwa ufanisi. Mwongozo huu unaweza kufanyiwa maboresho wakati wowote kulingana na mahitaji ili kukidhi malengo ya Serikali katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi.